**SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR**

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**

# HOTUBA YA WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

**MH. RIZIKI PEMBE JUMA (MBM)**

## KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA MWAKA WA FEDHA 2023/2024.

**MEI, 2023**

# YALIYOMO

YALIYOMO ........................................................ 1
MAELEZO YA VIFUPISHIO VYA MANENO.................. 2
1.0 UTANGULIZI ............................................... 3
2.0 MUUNDO NA MAJUKUMU YA WIZARA ............. 5
3.0 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2022-MACHI 2023 .... 6
a.Mapato yaliyokusanywa na Wizara kulingana na malengo yaliyowekwa .................................... 6
b. Changamoto na Mafanikio kwa kipindi cha Julai 2022 – Machi 2023 .................................. 6
c. Fedha iliyopatikana katika utekelezaji kwa kipindi cha Julai 2022 – Machi 2023................... 7
d. Utekelezaji wa Programu za Wizara kwa kipindi cha Julai 2022 - Machi 2023. .................. 8
4.0 PROGRAMU YA HIFADHI YA JAMII (PH0401) .... 10
4.1 Programu ndogo ya Hifadhi ya Jamii .............. 11
5.0 PROGRAMU YA URATIBU NA UENDESHAJI WA WIZARA (PH0402) .................................... 20
5.1 Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji..... 22
5.2 Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti........................................... 26
5.3 Programu ndogo ya Uratibu wa Wizara Ofisi Kuu Pemba ............................................... 28
6.0 PROGRAMU YA MAENDELEO YA JAMII NA JINSIA (PH0403)............................................. 29
7.0 UTEKELEZAJI WA MRADI KWA KIPINDI CHA JULAI 2022- MACHI 2023 ................................ 37

8.0 MWELEKEO WA BAJETI YA WIZARA KWA .
MWAKA 2023/2024 .......................................... 38
a.Vipaumbele vya Wizara kwa mwaka
2023/2024 .................................................. 38
b. Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara
kwa mwaka 2023/2024 .................................. 39
9.0.SHUGHULI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA
KWA MWAKA 2023/2024 ................................ 40
9.1 PROGRAMU YA HIFADHI YA JAMII
(PH0401) ................................................... 40
9.2 PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU
WA WIZARA (PH0402) .................................. 41
9.2.1Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji
(PH040201) ............................................... 41
9.2.2Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango,
Sera na Utafiti (PH040202) .......................... 42
9.2.3Programu ndogo ya Uratibu wa shughuli za
Wizara Pemba (PH040203) ........................... 43
9.3 PROGRAMU YA MAENDELEO YA JAMII NA
JINSIA (PH0403) ......................................... 43
10 SHUKRANI .................................................. 45
11 HITIMISHO .................................................. 48
11.1 MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA
FEDHA 2023/2024 ...................................... 48
VIAMBATISHO ................................................ 51

# MAELEZO YA VIFUPISHIO VYA MANENO

| | |
|---|---|
| CCM | Chama Cha Mapinduzi |
| DPP | Mkurugenzi wa Mashtaka |
| EU | European Union |
| GEF | Generation Equality Forum |
| IOM | International Organization for Migration |
| IPA | Institute of Public Administration |
| ITV | Independent Television |
| JKU | Jeshi la Kujenga Uchumi |
| JUWAZA | Jumuiya ya Wastaafu na Wazee Zanzibar |
| JUYAWAZA | Jumuiya Ya Wazee Zanzibar |
| KIU | Kampala International University |
| LSF | Legal Services Facilities |
| NPA-VAWC | National Plan of Action – Violence Against Women and Children |
| PBB | Performance Based Budget |
| PBZ | People's Bank of Zanzibar |
| PhD | Doctor of Phylosophy |
| SUZA | State University of Zanzibar |
| TAMWA | Tanzania Media Women Association |
| TBC | Tanzania Broadcasting Corporation |
| TIRA | Tanzania Insuarance Regulation Authority |
| THESODE | Theatre for Social Development |
| TRA | Tanzania Revenue Authority |
| UAE | Umoja wa Falme za Kiarabu |
| UNFPA | United Nations Population Fund |
| UNICEF | United Nations International Children's Emargency Fund |
| UNWOMEN | United Nation for Women |
| USAID | United State Agency for Internation Development |
| WHO | World Health Organization |

| | |
|---|---|
| ZACA | Zanzibar Children Association |
| ZAMWASO | Zanzibar Muslim Women Aids Support Organization |
| ZASO | Zanzibar Social Organization |
| ZASWA | Zanzibar Social Workers Association |
| ZBC | Zanzibar Broadcasting Corporation |
| ZC TV | Zanzibar Cable Television |
| ZPC | Shirika la Bandari Zanzibar |
| ZSSF | Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar |
| ZSTC | Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar |
| ZURA | Mamlaka ya Udhibiti wa Maji na Nishati Zanzibar |
| ZU | Zanzibar University |

## 1.0 UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha hotuba ya bajeti katika Baraza lako tukufu kwa ajili ya kupokea, kujadili na hatimaye kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

2. **Mheshimiwa Spika**, Kwanza kabisa naomba kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema aliyeumba mbingu na ardhi na vyote vilivyomo baina yake kwa kutujaalia uhai, uzima na afya njema hali iliyopelekea kukutana katika kikao hiki cha tatu cha kujadili bajeti tokea kuanza kwa shughuli za Baraza la 11 la Wawakilishi, Zanzibar. Aidha, natoa shukrani za pekee kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa **Dkt. Hussein Ali Mwinyi** kwa kuongoza nchi yetu ikiwa na amani na utulivu pamoja na juhudi kubwa anazozichukuwa kuhakikisha jamii ya Wazanzibari inakuwa na ustawi na maendeleo endelevu kupitia Uongozi wake wa busara na hekima. Pia, tunampongeza na kumshukuru kwa dhati kwa kuongeza kima cha pencheni kwa wazee wanufaika wa Pencheni Jamii kwa asilimia 150 pamoja na kuongeza kima cha pencheni kwa wastaafu.

3. **Mheshimiwa Spika**, Shukrani za dhati ziende kwa Makamo wa Kwanza wa Rais **Mheshimiwa Othman Masoud Othman** na Makamo wa Pili wa Rais **Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdullah** kwa kuweza kumsaidia na kumshauri Mheshimiwa Rais wa Zanzibar katika utekelezaji wa majukumu ya Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kutoa huduma bora kwa wananchi. Aidha, pongezi ziende kwao kwa kutuelekeza, kutuongoza na kutoa michango yao kwa maendeleo ya nchi yetu.

4. **Mheshimiwa Spika**, kwa moyo wangu wa dhati kabisa naomba kuchukuwa fursa hii kumpongeza mama yetu mpendwa mke wa Rais wa Zanzibar **Mama Mariam Mwinyi** Mwenyekiti wa Jumuiya ya "Zanzibar Maisha Bora Foundation" kwa kuwa sambamba na Wizara yangu kusaidia maendeleo ya wanawake, watoto na wazee kwa kasi ya maendeleo kupitia Uchumi wa Buluu kwa kuleta tija katika maendeleo ya wanawake, watoto na ustawi wa jamii kwa ujumla wake.

5. **Mheshimiwa Spika**, naomba pia nikupongeze wewe binafsi, Naibu Spika, Wenyeviti wa Baraza lako tukufu pamoja na wajumbe wa Kamati mbali mbali za Baraza kwa kufanya kazi zao kwa umakini na ueledi. Uongozi wenu unaendelea kuwa wenye hekima na busara katika uendeshaji na usimamizi wa majukumu ya Baraza hili katika upitishaji wa Makadirio na Matumizi ya sekta mbali mbali.

6. **Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa **Dkt. Samia Suluhu Hassan** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa kinara wa Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa Duniani (GEF). Aidha, Tanzania imechaguliwa kuwa mwenyeji na msimamizi wa Jukwaa hilo ambalo mkutano wake unatarajiwa kufanyika mwezi Septemba 2023 nchini Marekani, ambapo Mheshimiwa Rais ndiye mwenyeji wa Mkutano huo katika eneo namba mbili la Haki na Usawa wa Kiuchumi (Economic Justice and Rights).

7. **Mheshimiwa Spika**, Wizara inatambuwa na kuthamini mchango mkubwa wa wajumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi inayoongozwa na Mwenyekiti wake **Mheshimiwa Mohamed Ahmada Salum** na Makamo Mwenyekiti wake **Mheshimiwa Mwantatu Mbaraka Khamis** pamoja na wajumbe na makatibu wa Kamati kwa namna wanavyoshirikiana nasi katika kutekeleza majukumu yao kwa Wizara yangu, pia nashukuru sana kwa kuyapitia mapendekezo ya bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024 na kutupatia michango mingi ambayo imetuwezesha kuandaa hotuba hii na kuiwasilisha mbele ya Baraza hili tukufu.

## 2.0 MUUNDO NA MAJUKUMU YA WIZARA

**8.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, katika utekelezaji wa shughuli zake za kawaida zinatekelezwa kupitia Idara nne (4) ambazo ni; Idara ya Ustawi wa Jamii na Wazee, Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Ofisi Kuu Pemba, Idara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Pia, ina Vitengo sita (6) na Divisheni 14 ambazo utekelezaji wa majukumu yake unasimamiwa na Idara hizo.

**9.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto tokea kuanzishwa kwake Machi, 2022 imepangiwa kutekeleza majukumu yafuatayo: -

i. Kuweka mazingira bora ya Ustawi wa Jamii, Watoto, Wazee na kusimamia malipo ya Pencheni Jamii,
ii. Kuimarisha hifadhi ya wazee, utoaji wa misaada ya kiustawi kwa wananchi wanaoishi katika mazingira magumu zaidi;
iii. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera, Mipango, Tafiti, Ufuatiliaji na Tathmini ya shughuli za Wizara;
iv. Kusimamia maslahi ya rasilimali watu na nyenzo za utendaji kazi kwa uendeshaji na utoaji wa huduma bora, pamoja na kuhifadhi na kutunza kumbukumbu;

v. Kuimarisha mfumo wa hifadhi ya mtoto na kusimamia haki na wajibu wao; na
vi. Kuimarisha uratibu wa ufikiwaji wa usawa wa kijinsia na kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia.

10. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto ni miongoni mwa Taasisi za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ambayo inatumia mfumo wa bajeti wa kiprogramu (PBB) katika utekelezaji wa mpango kazi wa mwaka 2022/23. Wizara imetekeleza shughuli zake kupitia programu kuu tatu (3) na programu ndogo tatu (3) ambazo ni: -

i. Programu ya Hifadhi ya Jamii (PH0401)
ii. Programu ya Uratibu na Uendeshaji (PH0402)
- Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji (PH040201)
- Programu ndogo ya Uratibu wa Sera, Mipango na Utafiti (PH040202)
- Programu ndogo ya Uratibu wa shughuli za Wizara Pemba (PH040203)

iii. Programu ya Maendeleo ya Jamii na Jinsia (PH0403)

## 3.0 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2022 – MACHI 2023

### a. Mapato yaliyokusanywa na Wizara kulingana na malengo yaliyowekwa

11. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ilikadiriwa kukusanya kiasi cha **shilingi 15,000,000/-** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, hadi kufikia Machi 2023 Wizara imefanikiwa kukusanya kiasi cha **shilingi 5,200,000/-** sawa na **asilimia 34.7** ya makisio ya mapato hayo na zimewasilishwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

### b. Changamoto na Mafanikio kwa kipindi cha Julai 2022 – Machi 2023

12. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha utekelezaji wa Julai 2022 hadi Machi 2023, Wizara imekabiliana na changamoto zifuatazo: -

    i. Kuendelea kuwepo vitendo vya ukatili na udhalilishaji kwa wanawake na watoto,
    ii. Hali duni za maisha kiuchumi na kijamii kwa baadhi ya wanawake,
    iii. Ongezeko la utelekezaji na uwajibikaji mdogo kwa baadhi ya familia,
    iv. Uhaba wa vitendea kazi na vyombo vya usafiri,
    v. Jamii kutoitumia kwa usahihi nambari ya simu 116,

vi. Kuongezeka kwa watoto wanaokinzana na sheria.

13. **Mheshimiwa Spika**, Jitihada mbali mbali zimechukuliwa na Wizara katika kukabiliana na changamoto ili kupata ufumbuzi wake zikiwemo kuelimisha zaidi jamii kuhusiana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia na jinsi ya kuitumia vizuri na kwa usahihi simu nambari 116, kuendelea kuhamasisha na kuelimisha wanawake jinsi ya kuimarisha uzalishaji, kutafuta mitaji na mbinu za masoko pamoja na kufuatilia mnyororo wa thamani kwa bidhaa wanazozalisha. Aidha, suala la nyenzo za kutendea kazi linaendelea na taratibu za manunuzi. Pia, Wizara inaendelea kuongeza kasi ya kuelimisha jamii kuhusu malezi shirikishi, kufanya mageuzi ya kiprogramu na kuunganishwa na huduma za marekebisho ya maadili na tabia njema. Sambamba na kufanya mapitio na marekebisho ya Sheria ya Mtoto Nam. 6 ya mwaka 2011.

14. **Mheshimiwa Spika,** pamoja na changamoto zilizopo, lakini yapo baadhi ya mafanikio kadhaa yaliyopatikana katika sekta kwa kuzingatia utekelezaji wa Ahadi za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, maagizo ya viongozi wakuu, Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020-2025, Sera, Mipango ya Kitaifa na Kimataifa. Mafanikio hayo ni kama yafuatayo: -

i. Kuongezeka uelewa kwa jamii katika kujikinga na kuripoti matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia katika vyombo vya sheria,
ii. Kusimamia uratibu wa utoaji Pencheni Jamii,
iii. Kutoa msaada kwa watu wanaoishi katika mazingira magumu zaidi,
iv. Kuongezeka kwa utaalamu na ujuzi kwa wajasiriamali wanawake katika shughuli za ujasiriamali na uzalishaji,
v. Kuimarika kwa mashirikiano na Taasisi mbalimbali za ndani na nje katika uendeshaji wa shughuli za Wizara.

c. Fedha iliyopatikana katika utekelezaji kwa kipindi cha Julai 2022 – Machi 2023

15. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2022/23, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Fungu H04) ilikadiriwa kupata **shilingi 15,936,200,000/-** zikiwemo **shilingi 1,946,500,000/-** kwa ajili ya mishahara, **shilingi 10,229,100,000/-** kwa ajili ya kazi za uendeshaji wa ofisi, **shilingi 760,600,000/-** Ruzuku kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na **shilingi 3,000,000,000/-** kwa ajili kazi za mradi wa maendeleo.

16. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Machi 2023, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (H04) iliingiziwa jumla ya **shilingi 9,221,999,764/-** sawa na asilimia **58** ya makisio

ya bajeti ya mwaka 2022/23. Kati ya hizo **shilingi 6,608,157,530/-** sawa na asilimia **72** zilitumika kwa ajili ya uendeshaji sawa na asilimia **65** ya makisio ya bajeti, **shilingi 2,266,620,090/-** sawa na asilimia **25** zilitumika kwa ajili ya mishahara sawa na asilimia **116** ya makisio ya bajeti (Ongezeko hili la matumizi ya mishahara linatokana na kuongezeka kwa mishahara na watumishi ili kuongeza nguvu katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara). **Shilingi 220,009,344/-** ni asilimia **2** ya matumizi ambayo ni ruzuku kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na ni sawa na asilimia 29 ya makisio. Mwisho **shilingi 125,000,000/-** sawa na asilimia **1** kwa ajili ya kazi za mradi wa maendeleo sawa na asilimia **4** ya makisio. **(Kiambatisho nambari 1 kinatoa ufafanuzi).**

**d. Utekelezaji wa Programu za Wizara kwa kipindi cha Julai 2022 - Machi 2023.**

**17.** **Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo sasa naomba uniruhusu kutoa taarifa ya utekelezaji wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kwa kuzingatia malengo yaliyowekwa na vipaumbele vyake.

**18.** **Mheshimiwa Spika**, shughuli zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2022/2023 zilizingatia Sera, Sheria, mikakati ya Kitaifa na

Kimataifa, Ahadi za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Maelekezo ya Serikali pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi- CCM (2020-2025). Katika kipindi cha utekelezaji, Wizara imepata mafanikio mengi kutokana na shughuli zilizofanywa na Idara, vitengo na divisheni zilizopo kwa ajili ya kufikia malengo yaliyokusudiwa kwa mujibu wa shabaha na vipaumbele ambavyo vinagusa maeneo yafuatayo: -

i. Kuongeza nguvu katika usimamizi wa miradi ya maendeleo
ii. Kuimarisha nguvu kazi, kusimamia utendaji pamoja na kuandaa mazingira mazuri ya kazi,
iii. Kuimarisha mapambano dhidi ya vitendo vya ukatili kwa wanawake na watoto,
iv. Kuimarisha hifadhi ya jamii kwa wanaoishi katika mazingira magumu,

19. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha vipaumbele vilivyopangwa vimefikiwa, taarifa ya utekelezaji wa shughuli zilizopangwa zimeripotiwa kwa programu husika kama ifuatavyo: -

## 4.0 PROGRAMU YA HIFADHI YA JAMII (PH0401)

20. **Mheshimiwa Spika**, katika programu hii kuna programu ndogo moja (1) ambayo utekelezaji wa shughuli zake inatekelezwa kulingana na makadirio

ya fedha kwa mwaka wa fedha 2022/2023, programu ndogo hiyo ni Hifadhi ya Jamii.

### 4.1 Programu ndogo ya Hifadhi ya Jamii

**21.** **Mheshimiwa Spika**, Programu hii ina jukumu la kuratibu na kusimamia upatikanaji wa haki kwa makundi yenye mazingira magumu kwa kuimarisha mifumo ya hifadhi ya jamii na huduma kwa wazee, watoto na watu wanaoishi katika mazingira magumu zaidi ili kupunguza kiwango cha umasikini hapa Zanzibar.

**22.** **Mheshimiwa Spika**, shughuli za hifadhi ya jamii zinatekelezwa kwa kuzingatia mikakati ya Kitaifa na Kimataifa, Sheria ya Mtoto Nam.6 ya mwaka 2011, Sheria ya Fidia Nam.15 ya mwaka 1986 na marekebisho yake ya Sheria Nam. 5 ya mwaka 2005, Sheria ya Wazee Nam. 2 ya mwaka 2020 na Sera ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2014. Kwa mwaka wa fedha 2022/23, Programu hii ilitengewa **shilingi 13,442,555,010/-** sawa na asilimia 84.35, kati ya hizo **shilingi 10,442,555,010/-** zilitengwa kwa ajili ya shughuli za uendeshaji na **shilingi 3,000,000,000/-** zilitengwa kwa shughuli za mradi wa maendeleo.

**23.** **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Machi 2023, programu ya hifadhi ya jamii (PH0401) iliingiziwa jumla ya **shilingi 6,161,654,354/-** sawa na

asilimia 59.01 ya fedha ya shughuli za uendeshaji, kati ya hizo **shilingi 5,441,003,530/-** sawa na asilimia 88.30 zilitumika kwa Pencheni Jamii, **shilingi 595,650,855/-** sawa na asilimia **9.67** zilitumika kwa shughuli za kiofisi na **shilingi 125,000,000/-** sawa na asilimia **2.03** zilitumika kwa shughuli za kazi za miradi ya maendeleo.

**24.** **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 programu hii ilitengewa fedha kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kufanya ukarabati katika Makaazi ya Wazee Welezo na Sebleni;
ii. Kukamilisha ujenzi wa uzio katika Makaazi ya wazee Welezo;
iii. Kusimamia uendeshaji wa Mpango wa malipo ya Pensheni ya Jamii;
iv. Kutoa huduma za hifadhi na ustawi wa jamii kwa watu wenye mazingira magumu;
v. Kutayarisha mkakati wa mawasiliano ili kuimarisha mifumo ya familia na kupambana na vitendo vya ukatili kwa watoto.

**25.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara inaendelea na taratibu za manunuzi ya kupata mshauri elekezi pamoja na mkandarasi wa kufanya ukarabati katika Makaazi ya Wazee Sebleni na Limbani. Aidha, kwa ukarabati wa Welezo pamoja na uzio wake, Wizara imewasilisha ramani ya eneo la Welezo (site plan)

kwa Mshirika wa Maendeleo kutoka Umoja wa Nchi za Falme za Kiarabu (UAE) kwa kufadhili ujenzi wa kisasa wa makaazi ya wazee ambapo Serikali imeshatiliana saini mkataba wa ujenzi na mfadhili huyo.

26. **Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha huduma za hifadhi ya jamii zinaendelea, programu imeendelea kutoa huduma hizo kwa jamii kwa kuendeleza kuwatunza wazee waliopo kwenye makao ya Sebleni, Welezo na Limbani. Hadi kufikia Machi 2023, jumla ya Wazee 61 waliopo katika makaazi ya wazee Welezo 34 (wanawake 11 na wanaume 23), Sebleni 18 (wanawake 13 wanaume 05) na Limbani wazee 09 (wanawake 03 na wanaume 06), wanaendelea kupatiwa huduma za kiustawi ikiwa ni sehemu ya matunda ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikiwemo chakula, mavazi, malazi, matibabu na fedha za kujikimu. Aidha, tathmini imefanyika kwa wazee wanaohitaji kupata huduma za makaazi ya makao ya wazee Sebleni na Welezo ambapo wazee 3 walileta maombi yao kati ya hao wazee 2 ndio wenye sifa za kupatiwa huduma za makazi.

27. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2023 jumla ya wanafamilia 68 (36 Wanawake na 32 Wanaume) walipatiwa mafunzo juu ya umuhimu wa kuwatunza wazee na kuwapatia huduma muhimu kwa afya ya mwanadamu. Aidha, mafunzo

hayo yameongeza uelewa juu ya kuwakinga wazee na maradhi yasioambukiza, Wazee wengi wamegundulika kwamba wanasumbuliwa na maradhi yasiyoambukiza yakiwemo sindikizo la damu, kisukari, moyo na kensa.

28. **Mheshimiwa Spika**, katika kuendelea kuimarisha utoaji wa huduma za kiustawi, Wizara imetengeneza vitambulisho vya wazee 3,668 (1,497 wanawake, 2,171 wanaume) wamepatiwa vitambulisho ili kurahisisha upatikanaji wa huduma za kijamii ikiwemo huduma za usafiri, matibabu na msaada kwa wadau wanaoguswa na huduma za kiustawi. Aidha, uhakiki ulifanyika wa kuwatambua wazee wenye sifa za kutengenezewa vitambulisho ambapo wazee 25,000 (13,403 Unguja na 11,597 Pemba) na Wizara inaendelea na taratibu za kukamilisha vitambulisho hivyo.

29. **Mheshimiwa Spika**, Wizara iliadhimisha Siku ya Wazee Duniani ambayo hufanyika kila mwaka tarehe 01, Oktoba. Katika kuadhimisha siku hiyo, shughuli mbali mbali zilifanyika ikiwemo kupima afya za wazee, kufanya usafi wa maeneo ya wazee, kuelimisha jamii kupitia vyombo vya habari juu ya umuhimu wa kuwatunza wazee, na kilele cha shughuli hiyo kwa mwaka 2022/23, iliadhimishwa katika viwanja vya Hoteli ya la Verde mgeni Rasmi alikuwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

ambapo aliwakilishwa na Makamo wa Pili wa Rais Mhe. Hemed Suleiman Abdullah. Aidha, katika maadhimisho hayo alisisitiza umuhimu wa vitambulisho vya wazee katika upatikanaji wa huduma muhimu za jamii.

30. **Mheshimiwa Spika**, Uratibu wa mpango wa Pencheni Jamii kwa wazee waliofikia umri wa miaka 70 na kuendelea umefanyika. Hadi kufikia Machi 2023, jumla ya wanufaika wa mpango huu ni wazee 28,696 (17,076 Unguja na 11,620 Pemba). **Kiambatisho nambari 2 kinatoa ufafanuzi**.

31. **Mheshimiwa Spika**, uhakiki wa wazee unaendelea kufanyika kila mwezi kwa ajili ya kujiunga na mpango ambapo jumla ya wazee 1,074 wamehakikiwa kwa upande wa Unguja na 317 kwa upande wa Pemba. Aidha, mpango umesajili wazee wapya 1,727 (785 Unguja na 942 Pemba) ambao wanaendelea kupokea fedha zao kupitia mpango huu. **Kiambatisho nambari 3a na b vinatoa ufafanuzi.** Jumla ya wazee 1,711 (Unguja 1,111 na Pemba 600) wamefariki na kutolewa katika Mpango.

32. **Mheshimiwa Spika**, mafunzo kwa masheha wapya wa Wilaya ya Kaskazini “A” 44 (wanawake 02 wanaume 42) yalitolewa kwa lengo la kuwajengea uwezo katika suala la uendeshaji wa zoezi la kutoa huduma za Pencheni Jamii kwa wazee katika

shehia zao juu ya namna bora ya kusimamia na kufuatilia wazee ambao wamefikia umri wa miaka 70 na kuendelea. Aidha, mafunzo kama haya yanatarajiwa kutolewa hivi karibuni kwa masheha wa Wilaya ya Kaskazini “B”.

33. **Mheshimiwa Spika**, kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, ziara tano (5) zimefanyika kwa uongozi wa Wizara kutembelea vituo vinavyotumika kutoa huduma za Pencheni Jamii Unguja na Pemba ili kuhakikisha zoezi linaenda vizuri kiutendaji kama lilivyoratibiwa, kuangalia mapungufu na kutoa ushauri kutokana na uendeshaji wa zoezi hilo. Aidha, kujifunza kupitia kongamano kwa Nchi za Afrika iliyofanyika nchini Zambia kwa nchi zinazotoa huduma kama hizi (Cash Transfer) zimefanyika kwa nia ya kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma na uimarishaji wa mpango wa Pencheni Jamii.

34. **Mheshimiwa Spika**, kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Wizara ilipokea jumla ya malalamiko 457 (187 Unguja na 270 Pemba) yanayohusu ukiukwaji wa haki za watoto na mivutano ya malezi, ili kuhakikisha kuwa haki za watoto zinapatikana kwa mujibu wa sheria na taratibu zinazofaa. Malalamiko hayo yanahusisha matunzo ya watoto na mvutano wa malezi ambao huathiri zaidi watoto. **Kiambatisho nambari 4 kinatoa ufafanuzi.**

35. **Mheshimiwa Spika,** huduma za nyumba salama kwa wahanga wa vitendo vya udhalilishaji na ukatili wa kijinsia zimeendelea kutolewa, hadi kufikia Machi 2023, jumla ya wahanga 125, kati ya hao 1 mtu mzima na watoto 124 (wanawake 107 na wanaume 18) walipokelewa kwa ajili ya hifadhi ya muda kutokana na matukio mbali mbali ya udhalilishaji yaliyowakuta watoto. **Kiambatisho nambari 5 kinatoa ufafanuzi.**

36. **Mheshimiwa Spika**, huduma za kuwatunza watoto, hadi kufikia Machi 2023. Kituo cha marekebisho ya tabia kwa watoto wanaokinzana na sheria kiliweza kupokea watoto 08 (mwanamke 01 na wanaume 07). Takribani watoto wanaopatiwa huduma ya kurekebisha tabia ni wale waliofanya makosa yakiwemo; wizi, kukashifu, kutorosha, kubaka, kulawiti na kufanya shambulio la aibu au jaribio la kulawiti. Watoto hupatiwa taaluma ya mambo mbalimbali ikiwemo; stadi za maisha, ushauri nasaha, ufundi, ushoni, uchoraji, mafunzo ya kompyuta, sanaa ya maigizo, uchongaji wa mageti, ujasiriamali na michezo kama mpira na sarakasi.

37. **Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto Nam.6 ya mwaka 2011 kifungu cha 41, Wizara inapaswa kufanya tathmini ya kijamii kwa watoto wanaokinzana na sheria na hata wale wanaofanyiwa matukio ya ukatili na udhalilishaji. Kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023,

jumla ya kesi 99 (kesi za Jinai 45 na kesi za Madai 54) zilifunguliwa Mahakamani, kesi zilizotolewa hukumu ni 46. **Kiambatisho nambari 6 kinatoa ufafanuzi.**

38. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imefuatilia vituo vya kulelea watoto 11 vya binafsi vinavyotoa huduma za malezi kwa watoto 385 (wanawake 184 na wanaume 201). Pia Wizara inaendelea kukisimamia kituo chake cha kulelea watoto Mazizini chenye jumla ya watoto 26 (wanawake 13 na wanaume 13). **Kiambatisho nambari 7 kinatoa ufafanuzi.**

39. **Mheshimiwa Spika**, vituo vya Malezi ya kutwa (Day Care Centre) kwa watoto, hadi kufikia Machi 2023 Wizara imefanikiwa kuratibu na kufuatilia uendeshaji wa vituo 14 vya kutoa huduma za malezi hayo ambavyo vinatambulika kwa mujibu wa sheria na taratibu za Serikali.

40. **Mheshimiwa Spika**, huduma za Ustawi wa Jamii hadi kufikia Machi 2023, jumla ya familia 178 (108 Unguja na 70 Pemba) zinazoishi katika mazingira magumu zimepatiwa msaada wa **shilingi 30,000/-** kwa kaya kila mwezi. Sambamba na hilo, msaada wa akinamama 31 (23 Unguja na 8 Pemba) waliojifunguwa watoto pacha zaidi ya wawili nao pia wamepatiwa posho la **shilingi 30,000/-** kwa kila mmoja kwa mwezi, misaada hii ni kwa ajili ya kuweza kujikimu kimaisha.

41. **Mheshimiwa Spika**, madai ya fidia kwa waliopata ajali kazini, hadi kufikia Machi 2023, jumla ya madai 104 (64 Unguja na 40 Pemba) yenye thamani ya **shilingi 167,810,859/- (shilingi 110,574,852/-** Unguja na **shilingi 57,236,007/-** Pemba) yalipokelewa na kuchukuliwa hatua ya taratibu za kisheria kwa kuwasilishwa kwenye Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) kwa ajili ya hatua za malipo ambapo hadi mwezi wa Machi 2023 madai hayo yote yameshalipwa. Aidha, kesi mpya 19 za wafanyakazi ambao wamepata ajali kazini zimeripotiwa na tayari zimewasilishwa katika mfuko huo. Kwa sasa, madai ya fidia kwa wafanyakazi wa Serikali waliopata ajali kazini yatashughulikiwa na Mfuko huo.

42. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2023, Wizara imetoa huduma za mazishi ambapo jumla ya maiti 11 ambazo hazina ndugu/jamaa zimezikwa na Serikali, baadhi ya maiti hizo ni wazee waliokuwa wakiishi kwenye makao ya wazee Sebleni, Welezo na Limbani, maiti za hospitali kuu ya rufaa ya Mnazi Mmoja, ambao hawana jamaa au ndugu wa kuwazika pamoja na wageni wanaotoka nje ya nchi. Kutoka Kenya maiti moja ya kike na mzungu mmoja ambae hakutambulika nchi aliyotoka.

43. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imefanikiwa kuadhimisha Siku ya Ustawi wa Jamii Duniani ambapo kilele chake kilifanyika tarehe 21.03.2023 na Mgeni Rasmi alikuwa Makamo wa Pili wa Rais Mhe. Hemed Suleiman Abdullah, yenye lengo la kuimarisha huduma za kiustawi Zanzibar na ujumbe wa mwaka huu ulikuwa "Kuheshimu utofauti kupitia hatua za kijamii".

## 5.0 PROGRAMU YA URATIBU NA UENDESHAJI WA WIZARA (PH0402)

44. **Mheshimiwa Spika**, katika programu hii kuna jumla ya programu ndogo tatu (3) ambazo utekelezaji wa shughuli zake kila moja inatekeleza kulingana na makadirio ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya mwaka 2022/2023. Programu hizo ni Utawala na Uendeshaji, Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti na Uratibu wa shughuli za Wizara Ofisi Kuu Pemba.

45. **Mheshimiwa Spika**, programu hii inahusika na masuala ya rasilimali watu, ikiwemo ajira, kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia nafasi za masomo pamoja na stahiki zao. Aidha, ina jukumu la kuandaa na kusimamia sera, miongozo, mipango, tafiti na kuweka taarifa za ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa shughuli za Wizara. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, jumla ya **shilingi 1,135,490,530/-** sawa na asilimia **7.13** ya fedha

zilizotengwa kwenye bajeti ya Wizara kwa ajili ya shughuli zilizomo katika programu hii, ambapo **shilingi 653,787,500/-** kwa ajili ya Uratibu wa shughuli za Uendeshaji na Mipango Unguja na **shilingi 481,703,030/-** kwa ajili ya Uratibu na Uendeshaji Ofisi Kuu Pemba.

**46. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Machi 2023, jumla ya **shilingi 523,001,785/-** sawa na asilimia **46.06** ya fedha zilizotengwa zilipatikana kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kusomesha wafanyakazi katika fani mbali mbali pamoja na kutoa mafunzo kwa watendaji wa ngazi zote wanaoshughulikia matatizo ya kijamii nchini;
ii. Kufanya tafiti mbalimbali zinazohusu matatizo yanayoikabili jamii na kuweza kuondoa changamoto hizo hasa katika masuala ya udhalilishaji kwa wanawake na watoto;
iii. Kuendelea kufanya maboresho ya sheria na miongozo ambayo inatumiwa kutoa huduma katika jamii; na
iv. Kufanya programu za kijamii ili kujua hali halisi ya matatizo ya jamii na kuwezakuwafikia wale wote wanaotaka huduma za kiustawi.

47. **Mheshimiwa Spika**, katika uandaaji wa shughuli hizo ulizingatia programu kuu pekee, hata hivyo taaarifa ya utekelezaji wake umezingatia uasili wa majukumu ya kila programu ndogo husika.

## 5.1 Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji

48. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha utekelezaji Julai 2022 hadi kufikia Machi 2023, Wizara kupitia Idara ya Uendeshaji na Utumishi ina jukumu la kuhakikisha kuwa Wizara ina nyenzo za kutosha za kufanyia kazi, nyenzo hizo ni pamoja na rasilimali watu, fedha, majengo, usafiri, samani na vitendea kazi.

49. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Machi 2023, Wizara ina jumla ya wafanyakazi 310, kati ya hao Unguja 264(wanawake 168 na wanaume 96) na Pemba 46 (wanawake 24 wanaume 22). Aidha, wafanyakazi hao wamelipwa **shilingi 2,266,620,090/-** zaidi ya asilimia 116 zimetumika kwa ajili ya mishahara na bado marekebisho yanaendelea kufanyiwa kazi kwa baadhi yao. Pia, Wafanyakazi tisa (9) wamesharekebishiwa mishahara yao na 10 walibadilishwa kada kujaza maeneo yenye upungufu, malipo ya mshahara na malimbikizo yataanza kulipwa mwaka wa fedha 2023/24. Sambamba na hilo, Wafanyakazi 113 (99 Unguja na 14 Pemba) wamepata likizo zao za kawaida pamoja na malipo ya posho za likizo zao.

Aidha, Wizara ilishughulikia malalamiko matatu (3) ya wafanyakazi katika kupata stahiki zao na tayari wameshapatiwa ufumbuzi.

50. **Mheshimwa Spika**, wafanyakazi watatu (3) ambao wamefikia umri wa lazima wa kustaafu tayari wamestaafishwa kwa mujibu wataratibu za utumishi. Aidha, Wizara ilipokea wafanyakazi 35 (25 Unguja na 10 Pemba) kutoka taasisi nyengine ili kuja kuongeza nguvu ya utendaji, **kiambatisho nambari 8 kinatoa ufafanuzi**. Hadi kufikia Machi, 2023, Wizara imewapatia ruhusa za masomo na mafunzo ya muda mfupi kwa wafanyakazi ishirini na mbili (22) wakiwemo kumi na mbili (12) wa Vitengo wanane (8), wa Masjala wawili (2) kutoka Utumishi na Uendeshaji. Pia, Wizara imewapatia ruhusa za masomo ya nje na ndani ya nchi wafanyakazi wake kumi na mbili (12). Aidha, Wizara imepokea wanafunzi kumi na tano (15) wa mafunzo kwa vitendo kutoka vyuo ikiwemo Chuo cha Mwalimu Nyerere (10) na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) (5) pamoja na wanafunzi wanane (8) wanaofanya utafiti kutoka KIU (6), IPA (1) na Mwalimu Nyerere (1).

51. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Machi 2023 Wizara imefanya mapitio ya sheria na miongozo ambayo inatumiwa kutoa huduma katika jamii, tayari mikutano miwili (2) ya kukusanya maoni ya wadau kuhusu marekebisho ya Sheria ya Mtoto

Nam; 6 ya Mwaka 2011 imefanyika Unguja na Pemba kwa kushirikiana na Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar, ambapo ilihusisha Taasisi za Serikali na zisizo za Serikali zinazoshughulika na masuala ya watoto pamoja na jamii. Aidha, vikao kwa ajili ya uandishi wa marekebsiho ya sheria hiyo vimefanyika kwa kuyafanyia kazi maoni yote yaliyokusanywa kutoka kwa wadau.

52. **Mheshimiwa Spika**, Kanuni mbili zimeandaliwa na kupitiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Kanuni ya Makaazi ya Wazee na Pencheni Jamii na kusainiwa na Mhe: Waziri ili ziweze kutumika rasmi. Aidha, Rasimu za makubaliano ya mashirikiano (Memorandum of Understanding - MoU) baina ya Wizara na Taasisi tatu (3) yamefanyika ambayo yamehusisha Taasisi ya Daraja Foundation kwa ajili ya kuwapa ujuzi watoto wanaporejea kwenye familia zao, Ofisi ya Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar kwa ajili ya vyeti vya kuzaliwa na MEHATA kwa ajili ya uanzishaji wa kituo cha huduma za msaada wa kisaikolojia na kijamii kwa kushauriana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, makubaliano hayo yamesainiwa kwa ajili ya kushirikiana kutoa huduma kwa jamii.

53. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Machi 2023 Wizara imekodi sehemu ya jengo linalomilikiwa na Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC) liliopo Kinazini kwa ajili ya ofisi za Makao Makuu

ya sekta na limelipiwa shilingi 18,000,000/- kwa muda wa miezi sita (6). Aidha, baadhi ya vifaa na vitendea kazi vimenunuliwa vyenye thamani ya shilingi 82,200,800 kwa ajili ya wafanyakazi wa Wizara zikiwemo kompyuta, samani za ofisi, vifaa vya kuandikia na vifaa vyengine, bado utaratibu wa manunuzi unaendelea.

54. **Mheshimwa Spika**, hivi karibuni Wizara imeanzisha programu ya msaada na ushauri wa kisheria (legal aid clinic) kutokana na kuimarisha huduma za kijamii, programu hii inafanyika kila siku ya Jumatatu katika ofisi za Idara ya Ustawi wa Jamii na Wazee zilizopo Sebleni. Huduma zinazotolewa ni msaada wa ushauri na taaluma ya kisheria kwa mambo yote yanayowakabili wanajamii, jumla ya watu tisa (9) (7 wanawake na 2 wanaume) walipatiwa huduma za msaada wa kisheria.

55. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Machi 2023 tathmini (Survey) moja imefanyika kwa ajili ya vifaa vya TEHAMA vinavyotumika ndani ya sekta kwa lengo la kufanya matengenezo ya vifaa hivyo ili viweze kufanya kazi ya majaribio ya (Local Area Network - LAN) iliyopo Kinazini ili kuweza kutambua kama "cables" zilizopo zinaweza kuendelea kutumika katika utoaji wa huduma ya mtandao wa mkonga wa Serikali, pamoja na line ya simu za ndani. Aidha, muendelezo wa utengenezaji

wa barua pepe za watendaji wa Wizara umefanyika sambamba na mafunzo ya "file series" pamoja na uingizaji wa taarifa za Wizara katika mitandao ya kijamii.

## 5.2 Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti

**56.** **Mheshimiwa Spika**, programu ndogo hii inashughulika na kuandaa, kusimamia sera, miongozo, mipango ya sekta, tafiti na kukusanya taarifa za sekta zinazotokana na ufuatiliaji na tathmini na kufanya mapitio ya sera, miongozo na kanuni zinazohitajika kufanyiwa marekebisho.

**57.** **Mheshimiwa Spika**, katika kuendeleza mipango ya sekta, uratibu wa mafunzo umefanyika wa kuwajengea uwezo watendaji wa sekta juu ya kuandaa mipango ya maendeleo kupitia kazi za Idara katika utekelezaji wa majukumu ya kila divisheni, sambamba na kuwaelimisha wakuu wa vitengo na divisheni juu ya matumizi ya vifungu vilivyoainishwa katika bajeti iliyopitishwa mwaka 2022/2023 kwa matumizi sahihi ya vifungu hivyo.

**58.** **Mheshiwa Spika**, kwa kushirikiana na Taasisi ya Kijiji cha Watoto SOS mikutano miwili yenye kushirikisha wadau kutoka Serikali na Asasi zisizo za Serikali zimepitia rasimu ya Sera ya Mtoto ya mwaka 2019. Rasimu hiyo inaendelea na hatua ya kupitiwa na Wizara kabla ya kukamilika

kwake. Aidha, Mpango wa ufuatiliaji na tathmini umeanza kuandaliwa kwa mashirikiano na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu kwa hatua ya kutayarisha zana za kukusanyia taarifa/takwimu zinazohitajika ndani ya Wizara. Pia, uanzishaji wa mfumo wa ukusanyaji wa takwimu wa kesi za udhalilishaji kwa watoto (PRIMERO) kwa kushirikiana na Shirika la UNICEF pamoja na uanzishaji wa kanzi data (database) ya usajili wa malalamiko yanayowasilishwa Wizarani. Aidha, mafunzo ya wakufunzi 10 yamefanyika na kuweza kufundisha maafisa 32 maafisa Ustawi Wilaya na Mkoa kwa ajili ya matumizi ya mfumo huo.

59. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Machi 2023 Wizara ilifanya tathmini ya vikundi vya wajasiriamali wanawake 120 (72 Unguja na 48 Pemba) ambapo ilibainika kwamba asilimia 97 kati yao vimesajiliwa na asilimia 3 havikusajiliwa rasmi, shughuli kuu ambazo zinafanywa na vikundi hivyo ni ukulima wa mwani, ufugaji wa kuku, ushoni na kudarizi mashuka na mapazia, biashara ndogo ndogo, utengenezaji wa sabuni, mafuta, vyungu, ukulima wa mboga mboga, ufugaji nyuki na uvuvi. Taarifa kamili iliwasilishwa Wizara Nchi (OR) Kazi Uwekezaji na Uwezeshaji Kiuchumi ili kuweza kuviunganisha vikundi hivi kwenye Taasisi zinazotowa mikopo yenye masharti nafuu na kukuza uchumi wa mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla. **Kiambatisho nambari 9 kinafafanua**.

## 5.3 Programu ndogo ya Uratibu wa Wizara Ofisi Kuu Pemba

**60. Mheshimwa Spika**, Programu hii inashughulika na kusimamia shughuli zote za Wizara Pemba kwa kuzingatia sera, sheria, miongozo, mipango ya sekta pamoja na kusimamia matumizi na upatikanaji wa rasilimali kwa kutoa huduma bora.

**61. Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Idara ya Utumishi na Uendeshaji imekuwa ikijitahidi katika kuangalia ustawi wa wafanyakazi wake ambapo kwa kipindi cha Julai 2022-Machi 2023, Wizara iliwapatia likizo la kawaida wafanyakazi 14 kutoka Idara mbalimbali. Aidha, katika kuimarisha nguvu kazi ilipokea wafanyakazi 10 wa kada mbalimbali. Pamoja na hilo katika kipindi hiki cha utekelezaji, Ofisi Kuu Pemba imetengeneza ofisi zake na kufanya ununuzi wa samani za ofisi pamoja na kugharamia uendeshaji wa ofisi.

**62. Mheshimiwa Spika**, shughuli za mipango, sera na utafiti kwa kipindi cha Julai 2022 - Machi 2023, kupitia uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti imeweza kuandaa Bajeti (MTEF) kwa Idara ya Utumishi na Uendeshaji na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.

## 6.0 PROGRAMU YA MAENDELEO YA JAMII NA JINSIA (PH0403)

63. **Mheshimiwa Spika**, programu hii ina programu ndogo moja ambayo ni Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

64. **Mheshimiwa Spika**, programu hii inahusika na jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa haki za Wanawake, Wanaume na Watoto ikiwa ni pamoja na kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria zinazohusu Maendeleo ya Jamii wakiwemo Wanawake na Watoto pamoja na kuendeleza Wanawake hao kwa kuzingatia Mipango ya Kitaifa, Mikataba ya Kikanda na Kimataifa.

65. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 programu hii ilitengewa jumla ya **shilingi 1,358,154,460/-** sawa na asilimia **8.52** ya bajeti ya Wizara.

66. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Machi 2023, jumla ya **shilingi 523,001,785/-** sawa na asilimia 46.06 ya fedha zilizotengwa zilipatikana na zilitekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kujenga uwezo na ushiriki wa watoto katika mabaraza ya watoto;
ii. Kusimamia na kuendeleza juhudi za kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake;

iii. Kuendeleza mapambano dhidi ya vitendo vya ukatili na udhalilishaji kwa wanawake na watoto; na
iv. Kusimamia shughuli za maendeleo ya jamii.

**67. Mheshimiwa Spika**, ushiriki wa watoto katika mabaraza ya watoto, katika kipindi cha Julai 2022 - Machi 2023, Wizara kwa kushirikiana na Kijiji cha kulelea Watoto (SOS) kupitia mradi wa malezi mbadala ya kijamii imetoa mafunzo ya uongozi na jinsi ya kujikinga, kuandaa agenda za mabaraza, kuripoti vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia jumla ya mabaraza 107 (31 Magharibi A, 34 Magharibi B na Kati 42). Viongozi na wajumbe 93 wa mabaraza ya Watoto ya Shehia (42) za Wilaya ya Kati, Magharibi "B" (34) na wajumbe wa Bodi ya Ushauri ya Watoto (NCAB) 17 (10 Unguja na 7 Pemba). Aidha, kwa upande wa Pemba, mabaraza 9 yametembelewa (Ndagoni, Shungi, Shamiani, Michezani, Muwambe, Shumbageni, Jombwe Tumbe Mashariki, Tumbe Magharibi na Shumba mjini). Aidha, mabaraza mawili (Ndagoni na Shungi) yalipatiwa mafunzo ya kujenga uwezo kwa kushirikiana na NGOs ya KUKHAWA ambapo jumla ya watoto 10 wamepatiwa mafunzo (wanaume 5 na wanawake 5 kati ya watoto hao 2 walikuwa walemavu).

68. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Machi 2023, jumla ya waratibu wa wanawake na watoto wa Shehia 388 (259 Unguja na 129 Pemba) wamepatiwa posho la shilingi 60,000/- kila mmoja kwa kila robo mwaka kwa ajili ya ufuatiliaji wa matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa kijinsia katika maeneo yao pamoja na kuyafikisha katika vyombo vya sheria.

69. **Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha mifumo ya kuripoti matukio kupitia nambari 116, kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Wizara ilipokea jumla ya simu 2,912, simu 48 sawa na asilimia 2 zilihusu taarifa za ukiukwaji wa haki za watoto zikiwemo ukatili wa kingono (ubakaji na ulawiti), udhalilishaji wa kimwili, madai ya matunzo, utelekezwaji wa watoto na utoroshaji, kati ya hizo Simu 9 zilihusu malalamiko ya huduma kwa mtoto, elimu juu ya lishe bora, malezi pamoja na elimu kuhusu haki za watoto. Asilimia 98 ya simu hizo hazikuwa na taarifa maalum bali zilijumuisha simu za mzaha, malalamiko yaliyo nje ya huduma na simu zinazokatika bila ya kupokelewa na nyengine kukaa kimya. Simu zote rasmi sawa na asilimia 2 zimefanyiwa rufaa katika Taasisi za kutoa huduma ikiwemo Polisi, Ustawi wa Jamii na Wizara ya Elimu. **Kiambatisho nambari 10 kinatoa ufafanuzi**.

70. **Mheshimiwa Spika**, Wizara katika kuratibu na kufuatilia mapambano dhidi ya udhalilishaji kwa wanawake na Watoto, imeweza kusimamia kutoa taaluma katika maeneo mbali mbali ikiwemo Shehia 152 (Unguja 74 na Pemba 78), skuli 96 (Unguja 47 na Pemba 49), Madrasa 74 ( Unguja 46 na Pemba 28) kwa upande wa Khutba za Ijumaa 78 (Unguja 47 na Pemba 31). Lengo ni kujenga uelewa wa kujikinga na kuweza kuripoti matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia katika maeneo yao. **Kiambatisho nambari 11a &11b vinatoa ufafanuzi**

71. **Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 Wizara imefanikiwa kuunda Timu ya Wanaume wa Mabadiliko 35 (Male Champions) ya kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa Kijinsia ambapo jumla Madrasa 12 zimefikiwa na timu ya wanaume wa mabadiliko ya Wizara katika Mkoa wa Mjini Magharibi. Jumla ya wanufaika 1,586 walifikiwa kati ya hao 853 wanaume, 696 wanawake na walimu wa madrasa 37. Lengo ni kujenga uelewa wa namna ya kujikinga na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa Kijinsia kwa watoto na Jamii kwa ujumla. **Kiambatisho nambari 12 kinatoa ufafanuzi**.

72. **Mheshimiwa Spika**, katika harakati za kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji, Wizara imebaini kwamba wananchi wamekuwa

na uelewa kuhusu masuala mbali mbali ikiwemo dhana ya ukatili na udhalilishaji, aina, sababu na kubainisha maeneo hatarishi yanayopelekea vitendo vya ukatili na udhalilishaji vinavyotokea katika maeneo yao. Pia, wameweza kupanga mikakati yao ya kupambana na vitendo hivyo katika maeneo yao ikiwemo kuwazuwia watoto kutotembea nyakati za usiku, kuimarisha malezi ya pamoja, kuondoa viashiria hatarishi kama vile vichaka, maboma na kuimarisha ulinzi shirikishi ambapo wanajamii 11,070 (Wanaume 2,550 na Wanawake 8,520) walifikiwa.

73. **Mheshimiwa Spika**, uhamasishaji umefanyika kupitia mikusanyiko mbali mbali ya kijamii ikiwemo vikundi 19 vya mazoezi, Jumuiya ya Waendesha Bodaboda na Bajaji wa Unguja walielimishwa ambapo madereva 609 walifikiwa pamoja na madiko ya wavuvi. Aidha, kambi tatu za Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) za Unguja na Pemba (Kambi ya JKU Mtoni, Kambi ya JKU Bambi na Msaani Pemba) zenye vijana 3,296 (wanawake 495 na wanaume 2,801) walifikiwa.

74. **Mheshimiwa Spika**, kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2023 Wizara imefanikiwa kufanya mapitio ya Muongozo wa viongozi wa dini ili kuzingatia masuala mtambuka na kupunguza vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa Kijinsia. Aidha, Wizara imetoa mafunzo Unguja na Pemba kwa viongozi

wa dini, masheha na wadau mbalimbali juu ya kuzuwia vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia pamoja na ndoa za umri mdogo. Mafunzo hayo yalikuwa na lengo la kujenga uelewa wa makundi ya rika zote katika jamii ili waweze kushiriki katika mapambano dhidi ya vitendo vya ukatili na udhalilishaji.

75. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imefanya maadhimisho ya Kitaifa na Kimataifa ikiwemo siku 16 za wanaharakati wa kupinga vitendo vya ukatili na udhalilishaji Unguja na Pemba ambayo huadhimishwa kila ifikapo 25 Novemba hadi 10 Disemba. Ujumbe wa mwaka huu "Tuungane Kumaliza Ukatili na Udhalilishaji dhidi ya Wanawake na watoto". Ujumbe huu umelenga kuitaka Jamii katika ngazi zote kuunganisha nguvu kwa pamoja ili kutokomeza janga hili. Mgeni Rasmi alikuwa Mke wa Rais wa Zanzibar Mama Mariam Mwinyi na Mwenyekiti wa Zanzibar Maisha Bora Foundation. Vile vile katika kuadhimisha Siku ya Wanawake duniani, Wizara iliandaa maonesho ya wajasiriamali, matembezi ya hisani na mazoezi ya viungo, makongamano na mafunzo ya ujasiriamali kwa wanawake. Ujumbe wa mwaka huu "Wekeza ubunifu na matumizi sahihi ya teknolojia kwa usawa wa Kijinsia", jumla ya wajasiriamali wanawake na watoa huduma 96 kutoka taasisi za serikali na binafsi walishiriki.

76. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa Kutayarisha na kurusha vipindi vya Redio na TV 18 (12 Redio na 6 TV) pamoja na makala 2 zilitolewa katika gazeti la zanzibar leo,katika utoaji elimu hiyo mada zilizotayarishwa na zilitolewa ni ulinzi kwa watoto,haki za mtoto, usawa wa kijinsia ,ukatili na udhalilishaji wa kijinsia,vyombo vya habar vilivyotumika kurusha vipindi hivyo ni pamoja na ZBC TV, ITV, TBC na Zanzibar Cable (ZC), kwa upande wa Redio vipindi vilirushwa katika ZBC Redio, Bahari FM, Spice Fm, Redio Jamii, Redio Asalam na Redio noor.

77. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai 2022 hadi machi 2023 wizara imeendelea kutoa huduma za ushauri nasaha, msaada wa kisheria kwa wahanga wa vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa Kijinsia. Jumla ya wahanga aliohudumiwa kwa kipindi hiki ni kama ifuatavyo malalamiko 174 yalipokelewa na kufanyiwa kazi yakijumuisha migogoro ya ndoa 17, madai ya mali zilizochumwa kwa pamoja 3, madai ya mahari 4, madai ya talaka 1, mgogoro wa familia 3, mvutano wa malezi 24, matunzo ya watoto 51, kupigwa 9, kubakwa 8, kutorosha watoto 4, shambulio la kutaka kubakwa 1, kusingiziwa kutaka kubaka 1, marekebisho ya tabia za watoto 11, kulawiti 15, huduma za ujauzito 7, madai ya makaazi 5, mirathi 1, kukashifu 6, usafirishaji haramu 1 na kuibiwa kwa watoto 2. Kati ya malalako hayo 120 yameweza kupatiwa

ufumbuzi na wizara, 54 yamepatiwa rufaa katika taasisi nyengine (mahakama ya kadhi 12, Jeshi la Polisi 38, kamisheni ya wakfu na mali ya amana 1, Mahakama ya watoto 1, kituo cha huduma za sheria 1 na zafela 1.

78. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Machi 2023, mikutano 2 ya vikundi kazi vya wilaya 11 vya Wasaidizi wa sheria vya Wilaya zote za Unguja na Pemba zimefanikiwa kutoa elimu na kutoa msaada wa kisheria ambapo jumla ya matukio 143 yaliripotiwa na kupatiwa msaada wa kisheria (86 Unguja na 57 Pemba). **Kiambatisho nambari 13 kinatoa ufafanuzi**.

79. **Mheshimiwa Spika**, Wizara katika uwezeshaji wanawake kiuchumi imegharamia mafunzo ya wajasiriamali wanawake 42 (39 wa vikundi na 3 binafsi) juu ya usarifu wa matunda, mboga mboga pamoja na utengenezaji na uokaji wa mikate na keki katika chuo cha kukuzia na kulelea wajasiriamali Mbweni Zanzibar. Mafunzo hayo yamewawezesha wanavikundi hao kupata taaluma ya nadharia na vitendo pamoja na ujuzi wa kuzalisha bidhaa bora ili kuweza kujiajiri na kuajiri wengine. Pia, Wizara imevitembelea vikundi 17 katika wilaya 4 za Pemba (3 Chakechake, 3 Wete, 6 Mkoani na 5 Micheweni) ili kuona shughuli za uzalishaji, kubaini changamoto na kutoa miongozo na maelekezo.

80. **Mheshimiwa Spika**, aidha, katika kuratibu Ahadi za Kizazi Chenye Usawa Wizara imeweza kuwajengea uelewa waratibu wa Kisekta 35 kutoka sekta za umma juu ya Haki na Usawa wa Kiuchumi na maeneo yake ili kuweza kuingiza masuala ya Ahadi za Kizazi Chenye Usawa na masuala ya Usawa wa Kijinsia katika Bajeti zao za Kisekta na kuweza kuripoti kila robo mwaka. Itakumbukwa kwamba Mheshimiwa Dkt Samia Suluhu Hassan Raisi wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania aliridhia eneo nambari mbili katika jukwaa la Ahadi za Kizazi Chenye Usawa ambalo ni Haki na Usawa wa Kiuchumi.

## 7.0 UTEKELEZAJI WA MRADI KWA KIPINDI CHA JULAI 2022- MACHI 2023

81. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2022/23 Wizara ilipanga kutekeleza mradi wa maendeleo ambao ulipewa jina la Hifadhi ya Wazee, mradi huu una jumla ya shughuli kuu sita kwa ajili ya utekelezaji wake. Aidha, ulitengewa shilingi 3,000,000,000/- sawa na asilimia 18.83 ya makadirio ya bajeti.

82. **Mheshimiwa Spika**, kwa kipindi cha Julai 2022 – Machi 2023 jumla ya shilingi 125,000,000/- sawa na asilimia 4.17 ya fedha iliyotengwa imepatikana kwa ajili ya kutengeza vitambulisho vya wazee ili kuwasaidia upatikanaji wa huduma. Aidha,

shughuli nyengine zilizotarajiwa kutekelezwa ni pamoja ujenzi wa uzio wa makazi ya wazee Welezo, ukarabati wa majengo ya Sebleni, kununua samani za nyumba za wazee, ununuzi wa gari la Pencheni Jamii na kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa kuwatunza wazee.

## 8.0 MWELEKEO WA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2023/2024

### a. Vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2023/2024

83. **Mheshimiwa Spika**, mwelekeo wa utekelezaji wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka wa fedha 2023/2024 umezingatia maelekezo ya Awamu ya nane (8) katika kuimarisha utoaji wa huduma unaoendana na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM 2020-2025). Hivyo Wizara inaendelea kutekeleza maagizo yaliyotolewa katika matukio mbali mbali ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa.

84. **Mheshimiwa Spika**, kufuatia maamuzi ya Serikali, Wizara itahakikisha kwamba huduma zinaendelea kuimarishwa pamoja na kutia nguvu zaidi kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia na kustawisha jamii. Kwa mukhtadha huo, vipaumbele vya Wizara vimezingatia Mpango Mkakati wa Wizara 2023/2026, Mikakati ya Kitaifa na Kimataifa, Dira ya Maendeleo ya 2050, Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar 2021-2026,

Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020-2025 na maagizo ya Serikali. Vipaumbele hivyo vinagusa maeneo yafuatayo: -

i. Kuimarisha uratibu wa mapambano dhidi ya vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto;
ii. Kuimarisha nguvu kazi katika utendaji, sera, tafiti, miongozo, sheria, kanuni, pamoja na kuandaa mazingira mazuri ya kazi;
iii. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Ahadi za Nchi za Kizazi Chenye Usawa na uwezeshaji wanawake kiuchumi
iv. Kuimarisha Hifadhi ya Jamii, Wazee, Watoto na wanaoishi katika mazingira magumu; na
v. Kuratibu na kusimamia huduma za Pencheni Jamii.

**b. Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka 2023/2024**

**85. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imekadiriwa kukusanya jumla ya **shilingi 20,000,000/-** kuchangia mfuko Mkuu wa Serikali, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara imekadiriwa kutumia jumla ya **shilingi 9,887,311,000/-** kati ya fedha hizo **shilingi 7,170,000,000/-** sawa na asilimia **72.52** mchango wa Serikali na **shilingi 580,990,000/-**

sawa na asilimia 5.87 ruzuku kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Fedha za miradi ni **shilingi 2,136,321,000/- (Serikali shilingi 1,500,000,000/-** na Washirika wa Maendeleo **shilingi 636,321,000/-)** sawa na asilimia **21.61.**

**c. Mwelekeo wa Matumizi kwa Programu**

86. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ili kufikia malengo, mikakati mbalimbali itatekelezwa kuhakikisha utekelezaji wa shughuli zilizopangwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024 zinafanikiwa kupitia programu kuu na ndogo za Wizara.

## 9.0 SHUGHULI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KWA MWAKA 2023/2024

87. **Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha vipaumbele vilivyoainishwa hapo awali vinafikiwa, Wizara itatekeleza shughuli zilizopangwa kupitia programu husika kama ifuatavyo: -

### 9.1 PROGRAMU YA HIFADHI YA JAMII (PH0401)

88. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara imetenga shilingi 2,596,974,000/- sawa na asilimia 26.27 ya bajeti ya Wizara kwa ajili ya kutekeleza shughuli kuu zilizopangwa katika programu hii, ambapo **shilingi**

**1,500,000,000/-** kwa ajili ya mradi wa maendeleo na shilingi 1,096,974,000/- kwa ajili ya kutekeleza shughuli zilizopangwa na programu hii ambazo ni: -

i. Kuendelea kufanya ukarabati katika makaazi ya wazee Sebleni na Limbani;
ii. Kununua samani za makaazi ya wazee Sebleni na Limbani; na
iii. Kutoa huduma za hifadhi na ustawi wa jamii kwa watu wenye mazingira magumu zaidi.

## 9.2 PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA (PH0402)

**89. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara imetenga s**hilingi 5,648,868,500/-** sawa na asilimia **57** ya bajeti ya Wizara kwa ajili ya shughuli zilizomo katika programu hii. Ambapo **shilingi 3,170,000,000** kwa ajili ya mishahara, **shilingi 1,728,868,500/-** kwa ajili ya matumizi ya kiofisi Unguja na **shilingi 750,000,000/-** kwa ajili ya Afisi ya Uratibu na Uendeshaji Pemba.

### 9.2.1 Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji (PH040201)

**90. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara imepanga kutumia **shilingi 1,347,353,500/-** sawa asilimia **23.85** ya bajeti

ya fedha za programu hii kwa ajili ya shughuli zilizomo katika programu ndogo. Shughuli zitakazotekelezwa pamoja na:

i. Kuendelea kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Wizara;
ii. Kununua nyenzo pamoja na vifaa vya Wizara;
iii. Kuendelea kufanya mapitio na kurekebisha sheria, miongozo na kanuni za Wizara; na
iv. Kuendelea kuweka mazingira mazuri kwa wafanyakazi pamoja na kuwapatia maslahi yao.

### 9.2.2 Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti (PH040202)

91. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara imepanga kutumia **shilingi 381,515,000/-** sawa asilimia **6.78** ya bajeti ya fedha za programu hii kwa ajili ya shughuli zilizomo katika programu ndogo hii. Shughuli zitakazotekelezwa pamoja na:

i. Kufanya mapitio ya Sera, Kanuni na Miongozo inayohitaji kufanyiwa marekebisho;
ii. Kuratibu mipango, ripoti za utekelezaji, tafiti na chambuzi za kisekta na kuratibu shughuli za miradi ya maendeleo; na
iii. Kukusanya na kuchakata takwimu za kisekta, matukio ya udhalilishaji na ustawi wa jamii pamoja na kuziwasilisha kwa wadau.

### 9.2.3 Programu ndogo ya Uratibu wa shughuli za Wizara Pemba (PH040203)

92. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara imepanga kutumia **shilingi 750,000,000/-** sawa na asilimia **13.34** ya bajeti ya fedha za programu hii kwa ajili ya shughuli zilizomo katika programu ndogo hii. Shughuli zitakazotekelezwa pamoja na:

i. Kuratibu na kusimamia shughuli za utumishi na uendeshaji Ofisi Kuu Pemba;
ii. Kuendelea kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Wizara, Pemba;
iii. Kuendelea kuratibu na kusimamia sera, sheria, miongozo na kanuni za Wizara;
iv. Kuratibu na kuhamasisha jamii juu ya kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto; na
v. Kuendelea kuweka mazingira mazuri kwa wafanyakazi pamoja na kuwapatia maslahi yao.

## 9.3 PROGRAMU YA MAENDELEO YA JAMII NA JINSI (PH0403)

93. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara imetenga **shilingi 1,641,468,500/-** sawa na asilimia **17** ya bajeti ya Wizara kwa ajili ya shughuli zilizomo katika programu hii. Kati ya hizo, **shilingi 564,157,500/-**

mchango wa Serikali, **shilingi 1,077,311,000/-** ruzuku za Washirika wa Maendeleo kwa shughuli za uendeshaji na mradi wa Kupinga Ukatili na Udhalilishaji na Kubadilisha Wanawake kuingia kwenye nafasi za Uongozi. Shughuli zitakazotekelezwa kwa programu hii ni pamoja na: -

i. Kuandaa mpango kazi mpya wa kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto (NPA-VAWC 2023-2028);
ii. Kuhamasisha na kuelimisha jamii juu ya kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto katika ngazi zote;
iii. Kuandaa Sera ya Maendeleo ya Jamii pamoja na miongozo ya utoaji wa huduma za maendeleo ya jamii;
iv. Kuratibu na kuhamasisha utekelezaji wa Ahadi za Nchi juu ya Kizazi Chenye Usawa;
v. Kuratibu, kuwawezesha na kuwaunganisha wanawake na fursa mbalimbali;
vi. Kuratibu, kuwezesha na kuimarisha mabaraza ya watoto katika ngazi zote;
vii. Kuhamasisha na kuimarisha malezi ya pamoja; na
viii. Kutekeleza shughuli za kubadili wanawake kuingia kwenye nafasi za uongozi.

## 10 SHUKRANI

94. **Mheshimiwa Spika**, Mafanikio yaliyofikiwa yametokana na kuwepo mashirikiano mazuri na Taasisi za Serikali na zisizo za Serikali, mashirikiano ya Kitaifa na Kimataifa, Sekta binafsi na mtu mmoja mmoja. Wizara inatambua na kuthamini michango yao ya kifedha na kitaalamu wanayoitoa katika kufanikisha malengo ya Wizara. Itambuliwe kuwa Wizara hii ni mtambuka kwa Wizara zote na ni dhahiri kwamba dhana nzima ya utoaji wa huduma ikiwemo maendeleo ya jamii, kulinda ustawi wa jamii (wanawake, wanaume, wazee na Watoto), pamoja na kupambana na vitendo vyote vya ukatili na udhalilishaji kwa wanawake na watoto vinahitaji nguvu za pamoja. Hivyo basi, kwa niaba ya Wizara natoa shukrani za dhati kwa wote walioshirikiana nasi katika utekelezaji wa shughuli kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

95. **Mheshimiwa Spika**, shukrani za pekee ziende kwa Mama Mariam Mwinyi, Mke wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambae pia ni Mwenyekiti wa Zanzibar Maisha Bora Foundation kwa namna ya pekee katika kuguswa na masuala ya wanawake, wazee na watoto. Aidha, nawashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Ustawi wa Jamii wakiongozwa na Mwenyekiti Mheshimiwa Mohamed Ahmada Salum, kwa hakika wamekuwa mstari wa mbele katika kutoa michango na ushauri.

Naomba tuendelee kushirikiana ili kuimarisha ustawi wa Jamii na kuilinda jamii ya Wazanzibari.

96. **Meshimiwa Spika**, Napenda kutoa shukrani za dhati kwa uongozi wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto katika kuandaa na kukamilisha taarifa hii ya makadirio ya bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024, kwa kuanza na Naibu Waziri Mheshimiwa Anna Athanas Paul, Katibu Mkuu Ndugu: Abeida Rashid Abdallah, Afisa Mdhamini Ndugu: Hafidh Ali Mohamed Shoka, Mkurugenzi Mipango Sera na Utafiti, Ndugu: Bihindi Nassor Khatib, Mkurugenzi Uendeshaji na Utumishi, Ndugu: Salum Khamis Rashid, Mkurugenzi Ustawi wa Jamii na Wazee Ndugu: Hassan Ibrahim Suleiman, Mkurugenzi Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto Ndugu: Siti Abass Ali. Timu yote iliyoshiriki kuandaa taarifa ya Bajeti wakiwemo wakuu wa Divisheni, Vitengo, madereva pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara kwa ujumla wao. Bila ya kuwasahau Timu ya kusaidia Mapambano dhidi ya Ukatili na Udhalilishaji wakiwemo; masheha, waratibu wa wanawake na watoto wa shehia, viongozi wa dini, timu za wanaharakati, wasaidizi wa sheria pamoja na vituo vya mkono kwa mkono.

97. **Mheshimiwa Spika,** Naomba kutoa shukrani za pekee kwa Chama cha Mapinduzi (CCM) na Jumuiya zake kwa kusimamia vyema utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-2025, Washirika mbali mbali wa Maendeleo ambao kwa namna moja ama nyengine tunaendelea kushirikiana nao katika kuleta maendeleo kwa jamii, miongoni mwao ni, Ofisi za Ubalozi Mdogo wa China uliopo Zanzibar, UAE, EU, World Bank, UNICEF, UNFPA, UNWOMEN, WHO, HelpAge International, SOS, C-Sema, IOM, USAID, LSF, Action Aid, Save the Children, Step Up Foundation, Nuru Foundation, Noah Foundation and Good People, PBZ, ZURA, TRA, TIRA, Shirika la Bandari Zanzibar (ZPC), DPP, Mahakama, Jeshi la Polisi, Afisi ya Mtakuwimu Mkuu wa Serikal, SUZA, ZU, Mabaraza ya Wazee, JUWAZA, JUYAWAZA, TAMWA, ZASWA, ZAMWASO, ZASO, ZACA, Park Hayatt Hotel, THESODE, Zanzibar Maisha Bora Foundation, Daraja Foundation, Asma Mwinyi Foundation, Asalam Foundation, Sino youth Africa, Zanzibar Vijana Vision Group, Smile for Community na Vyuo Vikuu kwa ujumla. Pia nawashukuru wale wote ambao sikuwataja katika taarifa hii naomba watambue kuwa mchango wao tunauthamini sana.

## 11 HITIMISHO

### 11.1 MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

98. **Mheshimiwa Spika**, naomba wajumbe wa Baraza lako tukufu waipokee taarifa hii ya mapendekezo ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024 waijadili, waichangie kwa uwazi na hatimaye wakubali mapendekezo ya **shilingi 9,887,311,000/-** kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Fungu H04); Kati ya hizo **shilingi 3,170,000,000/-** kwa ajili ya mishahara, **shilingi 4,580,990,000/-** kwa matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi na **shilingi 2,136,321,000/-** kwa kazi za miradi ya maendeleo. **Kiambatisho nambari 14 kinatoa ufafanuzi.**

99. **Mheshimiwa Spika**, naomba kamati yako hii, ipokee makadirio ya mapato **shilingi 20,000,000/-** kwa fungu la Wizara (H04), kutoka vyanzo vya ukusanyaji wa mapato kwa ajili ya kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali.

100. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.



**RIZIKI PEMBE JUMA (MBM)**

**WAZIRI**

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO ZANZIBAR.**

# KIAMBATISHO

# VIAMBATISHO

Kiambatisho nambari1: Muhtasari wa Makisio na Matumizi Halisi pamoja na asilimia zao kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Julai, 2022- Machi 2023)

| Na | Shughuli | Makisio ya Bajeti | Halisi Kilichotumika | Asilimia ya Makisio kwa Halisi | Asilimia ya fedha iliyotumika kwa shughuli |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Kazi za Uendeshaji | 10,229,100,000 | 6,608,157,530 | 65 | 72 |
| 2. | Mishahara | 1,946,500,000 | 2,266,620,090 | 116 | 25 |
| 3. | Ruzuku za Washirika | 760,600,000 | 220,009,344 | 29 | 2 |
| 4. | Mradi wa maendeleo | 3,000,000,000 | 125,000,000 | 4 | 1 |
| | Jumla | 15,936,200,000 | 9,221,999,764 | 58 | 100 |

Chanzo: WMJJWW, 2022/23

**Kiambatisho nambari 2 Idadi ya wazee waliolipwa na Mpango wa Pecheni Jamii hadi kufikia Machi 2023**

| WILAYA | WANAUME | WANAWAKE | JUMLA |
|---|---|---|---|
| Kaskazini A | 1,496 | 2,290 | **3,786** |
| Kaskazini B | 711 | 1,060 | **1,771** |
| Kati | 809 | 1,019 | **1,828** |
| Kusini | 440 | 696 | **1,136** |
| Magharibi A | 658 | 1,012 | **1,670** |
| Magharibi B | 870 | 1,187 | **2,057** |
| Mjini | 2,193 | 2,635 | **4,828** |
| **Unguja** | **7,177** | **9,899** | **17,076** |
| Mkoani | 1,130 | 1,517 | **2,647** |
| Chake chake | 1,240 | 1,679 | **2,919** |
| Wete | 1,415 | 2,075 | **3,490** |
| Micheweni | 1,080 | 1,484 | **2,564** |
| **Pemba** | **4,865** | **6,755** | **11,620** |
| **JUMLA KUU** | **12,042** | **16,654** | **28,696** |

Chanzo: WMJJWW, 2022/23

Kiambatisho nambari 3a:  Wazee wapya waliosajiliwa Julai 2022 hadi Machi 2023

| UNGUJA | | |
|---|---|---|
| Na | WILAYA | IDADI YA WAZEE WAPYA |
| 1 | MAGHARIBI A | 90 |
| 2 | MAGHARIBI B | 122 |
| 3 | MJINI | 301 |
| 4 | KATI | 68 |
| 5 | KUSINI | 62 |
| 6 | KASKAZINI A | 69 |
| 7 | KASKAZINI B | 73 |
| | JUMLA | 785 |
| PEMBA | | |
| Na | WILAYA | IDADI YA WAZEE WAPYA |
| 1 | MKOANI | 220 |
| 2 | CHAKECHAKE | 240 |
| 3 | WETE | 235 |
| 4 | MICHEWENI | 247 |
| | JUMLA | 942 |
| JUMLA KUU | | 1,727 |

Chanzo: WMJJWW, 2022/23

Kiambatisho nambari 3b: Wazee waliofariki Julai, 2022 hadi Machi, 2023

| UNGUJA | | |
|---|---|---|
| Na | WILAYA | IDADI YA WAZEE WALIOFARIKI |
| 1 | MAGHARIBI A | 117 |
| 2 | MAGHARIBI B | 108 |
| 3 | MJINI | 288 |
| 4 | KATI | 119 |
| 5 | KUSINI | 91 |
| 6 | KASKAZINI A | 231 |
| 7 | KASKAZINI B | 157 |
| | JUMLA | 1,111 |
| PEMBA | | |
| Na | WILAYA | IDADI YA WAZEE WALIOFARIKI |
| 1 | MKOANI | 155 |
| 2 | CHAKECHAKE | 131 |
| 3 | WETE | 201 |
| 4 | MICHEWENI | 113 |
| | JUMLA | 600 |
| JUMLA KUU | | 1,711 |

Chanzo: WMJJWW, 2022/23

Kiambatisho nambari 4: Malalamiko ya Hifadhi ya Mtoto

| Na. | UNGUJA | | | | PEMBA | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Malalamiko | Idadi | Ufumbuzi | Rufaa | Idadi | Ufumbuzi | Rufaa |
| 1. | Kunyimwa matunzo | 127 | 57 | 17 | 181 | 122 | 03 |
| 2. | Mvutano wa malezi | 60 | 32 | 12 | 89 | 68 | 6 |

Chanzo: WMJJWW, 2022/23

Kiambatisho nambari 5: Kesi za watoto wa nyumba salama

| AINA YA TATIZO | | JINSIA | | UMRI | JUMLA NDOGO |
|---|---|---|---|---|---|
| Nam. | | KE | ME | | |
| 1. | USAFIRISHAJI HARAMU | 115 | 2 | 13-17 | 115 |
| 2. | KUPOTEA | 4 | - | 11-14 | 4 |
| 3. | KUTESWA | 1 | 1 | 11-13 | 2 |
| 4. | MVUTANO WA MALEZI | 1 | 1 | 16-18 | 2 |
| 5. | KUTELEKEZWA | 1 | - | 10 | 1 |
| | JUMLA KUU | | | | 124 |

Chanzo: WMJJWW, 2022/23

## Kiambatisha nambari 6 : Kesi Za Mahakama Ya Watoto

| MWAKA | MWEZI | KESI | ZILIZOFUNGULIWA | AINA YA KOSA | | | | | | | | | ZILIZOHUKUMIWA | ZINAZOENDELEA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | KINYUME NA MAUMBILE | MVUTANO WA MALEZI | MADAI YA MATUNZO | KULAWITI | KUTOROSHA | KUKASHIFU | WIZI WA KUTUMIA NGUVU | SHAMBULIO | KUBAKA | | |
| 2022 | Jul | JINAI | 7 | 2(1) | | | 1(1) | 2(1) | | - | 2(2) | - | 5 | |
| | | MADAI | 6 | | 4 | 2 | | | | | | | 0 | |
| | | | | | | | | | | | | | | |
| | Ag | JINAI | 9 | 2(1) | | | | 3 (1) | 1 | 1 | 1 | 1 (1) | 3 | |
| | | MADAI | 7 | | 3(2) | 4(2) | | | | | | | 4 | |
| | | | | | | | | | | | | | | |
| | Sep | JINAI | 6 | 1(1) | - | - | - | - | - | 2(1) | 3(2) | - | 4 | |
| | | MADAI | 4 | | 2 | 2(2) | | | | | | | 2 | |
| | | | | | | | | | | | | | | |
| | Okt | MADAI | 4 | | 1 | 3(1) | | - | - | | | - | 1 | |
| | | JINAI | 3 | | | | | | | 1(1) | | 2(2) | 3 | |
| | | | | | | | | | | | | | | |
| | Nov | MADAI | 7 | | 4(2) | 3(1) | | | | | | | 3 | |
| | | JINAI | 5 | - | | | - | - | - | - | 4 | 1 | 0 | |
| | | | | | | | | | | | | | | |
| | Dis | MADAI | 5 | | 1 | 4 | | | | | | | 0 | |

| | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2023 | | | | | | | | | | | | | | |
| | Jan | JINAI | 8 | | | | 1(1) | | 3 | 2 | 1 | 1(1) | 2 | |
| | | MADAI | 7 | | 4(1) | 3(2) | | | | | | | 3 | |
| | | | | | | | | | | | | | | |
| | Feb | MADAI | 8 | | 5(4) | 3(2) | | | | | | | 6 | |
| | | JINAI | 3 | | | | | 1 | | | | 2(2) | 2 | |
| | | | | | | | | | | | | | | |
| | Ma | MADAI | 6 | | 2(2) | 4(3) | | | | | | | 5 | |
| | | JINAI | 4 | | | | | | 1(1) | 1 | | 2(2) | 3 | |
| JUMLA YA KESI ZILIZOFUNGULIWA | | | 99 | | | | JUMLA YA KESI ZILIZOHUKUMIWA | | | | | | 46 | |
| | | | | 2 | 15 | 15 | - | 4 | 4 | 5 | 7 | 1 | | 53 |
| | | | | JINAI | MADAI | MADAI | JINAI | JINAI | JINAI | JINAI | JINAI | JINAI | | |

Chanzo: WMJJWW, 2022/23

Kiambatisho nambari 7: Orodha ya vituo vya kulea watoto yatima Zanzibar.

| NO | JINA LA KITUO | KE | ME | IDADI YA WATOTO | SEHEMU KILIOPO | SIMU | NAMBA ZA KIBALI | KIBALI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 01 | MAZIZINI | 13 | 13 | 26 | MAZIZINI | 0772142482 | | |
| 02 | FATMA HOUSE | 18 | 25 | 43 | JUMBI | 0778499993 | 01 | Ndio |
| 03 | KIDUNDO ORPHANAGE CENTRE | 10 | 15 | 25 | TUNGUU | 0777487666 | 02 | Ndio |
| 04 | S.O.S | 41 | 34 | 75 | MOMBASA | 0655429022 | 03 | Ndio |
| 05 | DARUL-AHBAB/PEMBA | 00 | 50 | 50 | MICHEWENI/PEMBA | 0777462483 | 04 | Ndio |
| 06 | SAKINA GIRLS HOME | 20 | 00 | 20 | JUMBI | 0774868962 | 05 | Ndio |
| 07 | SALIM TURKEY FOUNDATION | 24 | 00 | 24 | KANDWI | 0777777371 | 06 | Ndio |
| 08 | ASSALAM ORPHANAGE CENTRE | 11 | 25 | 36 | MPENDAE | 0778433962 | 07 | Ndio |
| 09 | ZASO CHILDREN'S HOME | 19 | 24 | 43 | FUONI MAMBOSASA | 0655207441 | 08 | Ndio |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 10 | AL-NASSER FOUNDATION | 00 | 00 | 00 | JUMBI | 0676717296 | 09 | Ndio |
| 11 | AL- MAFUT FOUNDATION | 35 | 20 | 55 | TUNGUU/KIBELE | 0776042214 | 10 | Ndio |
| 12 | AMANI FOUNDATION | 06 | 08 | 14 | MPENDAE | 0717052598 | | |
| | JUMLA KUU | 197 | 214 | 411 | | | 10 | |

Chanzo: WMJJWW, 2022/23


Kiambatisho nambari 8: Wafanyakazi waliopokelewa na kada zao

| Na | UNGUJA | | PEMBA | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| | KADA | IDADI | IDADI | |
| 1. | Afisa Manunuzi | 3 | 2 | 5 |
| 2. | Afisa Mipango | 1 | 2 | 3 |
| 3. | Afisa utumishi na uendeshaji | 2 | 1 | 3 |
| 4. | Uhasibu | 2 | 1 | 3 |
| 5. | Mshika fedha | 0 | 1 | 1 |
| 6. | Mkaguzi wa ndani | 2 | 1 | 3 |
| 7. | Katibu muhtasi | 3 | 1 | 4 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 8. | Afisa kumbukumbu | - | 1 | 1 |
| 9. | Afisa TEHAMA | 2 | - | 1 |
| 10 | Afisa habari | 1 | - | 1 |
| 11 | Afisa Sheria | 3 | - | 3 |
| 12 | Afisa ufuatiliaji na tathmin | 1 | - | 1 |
| 13 | Afisa maendeleo ya jamii na jinsia | 2 | - | 2 |
| 14 | Afisa ustawi | 1 | - | 1 |
| 15 | Wasaidizi wa viongozi | 3 | - | 3 |
| | JUMLA | 25 | 10 | 35 |

Chanzo: WMJJWW, 2022/23

**Kiambatisho namba 9: Vikundi vya wajasiriamali kwa Wilaya vilivyofanyiwa tathmin Julai-Machi 2022/23**




Chanzo: WMJJWW, 2022/23

**Kiambatisho nambari 10: Mawasiliano yaliyopokelewa katika huduma ya simu kwa Mtoto Zanzibar**

| S/N | AINA YA HUDUMA | IDADI YA SIMURASMI |
|---|---|---|
| 1. | HudumayaMtoto | 01 |
| 2. | Taarifayahudumazasimu | 01 |
| 3. | Taarifazaudhalilishaji | 01 |
| 4. | Ushaurinasaha (familia) | 01 |
| 5. | Matunzo | 01 |
| 6. | Taarifayahakiyamtoto | 04 |
| | JUMLA | 9 |

Chanzo: WMJJWW, 2022/23

Kiambatisho Nambari 11a: Uelimishaji Julai 2022 – Machi 2023

| S/NO | MAENEO YALIYOFIKIWA UNGUJA | IDADI |
|---|---|---|
| | UNGUJA | |
| 1 | Madrasa | 46 |
| 2 | Shehia | 74 |
| 3 | Skuli | 47 |
| 4 | Khutuba za Ijumaa | 47 |
| | JUMLA | 214 |
| | PEMBA | |
| 1 | Madrasa | 28 |
| 2 | Shehia | 78 |
| 3 | Skuli | 49 |
| 4 | Khutba za Ijumaa | 31 |
| | JUMLA | 186 |
| | Jumla kuu | 400 |

Chanzo: WMJJWW, 2022/23

**Kiambatisho 11b: Jedwali linaloonyesha Skuli, Madrasa na Shehia zilizofikiwa katika uelimishaji na uhamasishaji dhidi ya vitendo vya ukatili na udhalilishaji kwa kipindi July 2022- March 2023 Unguja**

| SHEHIA | SKULI | MADRASA | KHUTBA |
|---|---|---|---|
| Shehia ya Kwaalinatu, Jang'ombe Urusi, Shehia ya K/hewa bondeni, Shehia ya Mto wa pwani, Shehia ya Mkwajuni, Shehia ya Chaani Kubwa, Shehia ya Upenja, Shehia ya Kandwi, Shehia ya Donge Vijibweni, Shehia ya Donge Mnyimbi, Shehia ya Kitope, Shehia ya Bumbwini Makoba, Shehia ya Muyuni, Shehia ya Muungoni, Shehia ya Kitogani, Shehia ya Kidimni, J Shehia ya umbi, Shehia ya Kiboje Muembe shauri, Shehia ya Tomondo, Shehia ya Kijitoupele, Shehia ya Mnarani, Shehia ya Michikichini, Shehia | Potoa Msingi, Pale Msingi, Mkokotoni Msingi, Chuo cha Amali Mkokotoni, Mbuyu Maji Msingi, Hassnuu Makame Sekondari, Makunduchi Sekondari, Kiongoni Msingi, Chuo cha Utalii Jambiani, Memon Academy Msingi na Sekondari, Forodhani Sekondari, Unique Msingi, Pangatupu Msingi, Kikungwi Msingi, Mama Samia Msingi, Fuoni Msingi na Sekondari, AboudJumbe, Maungani Msingi, Chukwani Msingi na Chuo cha | MadrastAlshiaa, Madrsat Maryam, Madrasat Tajweed Madrsatul Swiratul-Janna, Madrasatu taqwa, Madrasatul Zawiyatul Islamiyya, Madrasatul Muhtabiina, Madrasatul Maamuur Madrasat Jawhari Madrasa ya kina mama nungwi, Madrasat Nuurul Atfali Madrasat Liman Madrasat Dhuriyat Madrasat Jauhar Madrasat Dhuriyyat Islamiya Madrasa Alzuhdi-Koani, Madrasat Arahman Kitumba | Msikiti wa ijumaa Kandwi Msikiti wa mto wa Pwani Msikiti wa Ijuaa Shangani Msikiti wa ijumaa Bwereu Msikiti wa Ijumaa Chaani Msikiti wa ijumaa uyagu Msikiti wa ijumaa Chaani Msikiti wa ijumaa Kidagoni Msikiti wa ijumaa Gomani Msikiti wa Mujitahidin Jongowe Msikiti wa Chwaka Msikiti Mkuu Jongowe |
| meya, Shehia ya Kizimkazi Shehia ya mkunguni, Shehia ya Koba Makunduchi, Shehia ya Michamvi, Shehia ya Kae Makunduchi, Shehia ya Kizimkazi Shehia ya Dimbani, Shehia ya Chuini, Shehia ya Masingini, Shehia ya Mwakaje, Shehia ya Kibweni, Shehia ya Kazole, Shehia ya Mchina, Shehia ya Pangeni Shehia ya Matetema, Shehia ya Donge Mtambile, Shehia ya Stesheni ya Zamani Mahonda Shehia ya Chwaka, Shehia ya Mtoni, Shehia ya Mwembeladu, Shehia ya Tazari, Kendwa, | Skuli ya Nassari Kae kuu Makunduchi Skuli ya Nassari Muungoni Skuli ya Kijichi Skuli ya Kizimbani Skuli ya Kihinani Skuli ya Secondari Ali Hassani, Skuli ya Kiwengwa, Skuli ya Mgambo, Skuli ya AL-Answar Bumbwini, Skuli ya Mwanakwerekwe, H, Skuli ya Mombasa, Skuli ya kwa Mchina, Skuli ya Msingi Maungani, | Madrasa Ansar Masingini, Madrasa Sifat Masingin, Madrasa Taalim Munduli, Madrsasa Noor Imani Munduli, Madrasa Makadara, Madrasa Nasiriya Matarumbeta, Madrassa Shamsi Karakana, Madrasa kwa Aliyani Mchangani, Madrassa Gulioni, | Mahonda Msikiti wa Donge Msikiti wa Bumbwini Msikiti wa Mwanakwerekwe Msikiti Imani Mtondooni Msikiti Alfallah Chukwani Masjid Ridhaa Migombani Masjid Taqwa Migombani Masjid Muhammad Jangómbe Urusi Masjid Raudha Kinuni, Masjid Irshad Kwarara, Msikiti wa Mahonda Hasara Roho, Msikiti wa Kibuteni, Msikiti wa Ijumaa Muyuni, Msikiti wa Ijumaa Makunduchi Masjid Ayoub Urusi, Masjid Al Adhahar, |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Amani, Kigunda, Mbuyu Tende, Kitumbo, Mgenihaji, | | | Masjid noor, Msikiti Mkubwa Mwembe Makumbi, Msikiti wa Ijumaa Chaani |

Chanzo: WMJJWW, 2022/23

**Kiambatisho Nambari 12: Madrasa Zilizotembelewa Na Timu Ya Wanaume Wa Mabadiliko Katika Mkoa Wa Mjini Magharibi**

| JINA LA WILAYU | S/NO | JINA LA MADRASA |
|---|---|---|
| Maghribi A | 1 | Iptidaiyah |
| | 2 | Qulatiniyah |
| | 3 | Shafiyah |
| | 4 | Rahmatullah |
| Magharibi B | 5 | Nassir |
| | 6 | Sirajil munira |
| | 7 | Nuruminallah, |
| | 8 | Twarriqa Jannah |
| Mjini | 9 | Swiratul Jannah |
| | 10 | Taqwa |
| | 11 | Zawiyatul-islamiya |
| | 12 | Muktadinah |
| JUMLA KUU YA MADRASA ZILIZOFIKIWA NI 12 | | |

Chanzo: WMJJWW, 2022/23

Kiambatisho nambari 13: Matukio yaliyopatiwa msaada wa kisheria

| Na | MATUKIO | UNGUJA | PEMBA | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Migogoro ya malezi ya mtoto | 25 | 6 | 31 |
| 2. | Shambulio la aibu | 13 | 11 | 24 |
| 3. | Kulawiti | 4 | 7 | 11 |
| 4. | Kubaka | 15 | 20 | 35 |
| 5. | Shambulio | 6 | 2 | 8 |
| 6. | Migogoro ya mahari | 7 | 1 | 8 |
| 7. | Usafirishaji haramu wa binadamu | 8 | - | 8 |
| 8. | Mimba za umri mdogo | 4 | 3 | 7 |
| 9. | Ndoa za mapema | 1 | 3 | 4 |
| 10. | Kutorosha | 2 | 2 | 4 |
| 11 | Kunajisi | 1 | 2 | 3 |
| | Jumla | 86 | 57 | 143 |

Chanzo: WMJJWW, 2022/23

**Kiambatisho nambari 14: Muhtasari wa Makisio ya Bajeti ya mwaka 2023/2024**

| Na | Shughuli | Makisio ya Bajeti(Tzs) |
|---|---|---|
| 2. | Mishahara | 3,170,000,000.00 |
| 3. | Uendeshaji wa Ofisi<br>Serikali<br>UNFPA<br>UNCEF | <br>4,000,000,000.00<br>300,990,000.00<br>280,000,000.00 |
| 4. | Kazi za maendeleo:<br>Serikali<br>UNWOMEN | <br>1,500,000,000.00<br>636,321,000.00 |
| | Jumla | 9,887,311,000.00 |

Chanzo:(OR)FM, 2023/24